

- Ikiwa yamehifadhiwa ndani ya nyumba, tumia sehemu iliyoinuliwa au kwenye visiki ili kuzuia kuota kuvu.
- Tenga nafasi kutoka kwenye ukuta ili kuwezesha kukagua nafaka vizuri.
- Tia dawa tena baada ya miezi 6.



a) Mahindi safi

b) Mahindi yaliharibiwa na wadudu



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Kimondo, M.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Kabete

S.L.P. 14733-00800 Nairobi

Simu: 020 4444144

Baruapepe: cdnarl@iconet.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 18 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Utunzaji na uhifadhi wa nafaka ya mahindi



Utangulizi

Asilimia 80 ya mahindi yanayovunwa nchini Kenya huhifadhiwa kwenye ghala za nyumbani. Kati ya asilimai 20 hadi 30 ya mavuno hupotea katika miezi 6 iwapo hakuna hatua za kuzuia zinazochukuliwa. Hasara kubwa ni kutokana na wadudu, panya na magonjwa.

Wadudu wa mahindi yaliyowekwa ghalani

Wadudu

- Wadudu walao mahindi
- Wadudu wanaotoboa nafaka “scania”
- Nondo na mende.

Panya

- Panya wa nyumba na wa vichaka.

Viini vya magonjwa

- Kuota kuvu na ukungu.

Hatua za kukinga uharibifu ni pamoja na:

Kuvuna wakati ufaao

- Uvunaji ufanywe mahindi kavu yainamapo.



Mahindi kavu huinama

Kukausha vizuri

- Uvunaji wa mikono ufuatwe na ukaushaji kwenye sehemu zilizoinuliwa au hema zilizotandikwa.
- Hori zilizo wazi au vikapu vyenye mashimo. Baadaye, mahindi yabambuliwe na yatiwe dawa.

Usafi wa ghala

- Maghala yasafishwe ili kuondoa nafaka za awali.
- Dawa ipulizwe ili kuuwa wadudu wowote.

Kuzitibu nafaka

Nafaka ziwekwe dawa ya vumbi ya kuhifadhi kwa kiasi cha gramu 50 kwa kila kilo 90 zinazopatikana katika maduka ya kuuza madawa ya kilimo.

- Kifaa cha kupimia kiwango hiki kimefungwa pamoja na dawa.
- Nafaka ziwekwe kwenye mikeka na kuchanganywa vizuri na dawa ya vumbi kwa kutumia sepetul.



Kuchanganya vizuri kwa nafaka



Mahindi yamepakwa vizuri katika magunia baada ya kutibiwa

- Kibonge cha sufi pia chaweza kutumia kuchanganya nafaka.
- Kuanika juu pia husaidia kuondoa wadudu lakini ni lazima mtindo huu ufanikishwe kwa kuongezea dawa.
- Panya wadhibitiwe kwa kutumia paka, mitego au chambo.

Hoja za kukumbuka

- Sharti mahindi yakauke kabisa ili kuzuia kushambuliwa na ukungu.
- Mahindi yenye kiwango kikubwa cha unyevu hupunguza ufanikifu wa dawa.
- Mahindi yanapobambuliwa, yatiwe dawa na kuhifadhiwa katika magunia au vifaa vingine vigumu kama mapipa.
- Hamisha magunia haya hadi kwenye ghala na wazinge panya kwa kutumia paka au mitego ya panya.